

W a r e n o w a t i s h a W a n a n c h i N e w a l a

Mreno anawatisha sana wananchi wa Tanganyika ambao wanalima kwenye kingo za mto Ruvuma. Penginipo, ndege kutoka Ureno zinaruka kuvuka Tanganyika na kuruka chini chini sana na wananchi ambao kazi yao na mategemeo yao ni kilimo cha mpunga kando kando ya Ruvuma wanatishika sana na usalama wa maisha yao. **NGURUMO**

Dai hili lilitolewa na B w a n a Rafael Said Mjumbe wa Newala katika hotuba yake kujadili hotuba ya siasa ya Waziri wa Usalamu hapapa nchini. Bwana Saidi aliomba ikiwezekana Wizara iweke kikosi maalum cha kulinda vema mpaka wa Tanganyika na Ureno.

Akifafanua zaidi juu ya dai lake, Bwana Saidi alisema mnamo tarehe 5 ya mwezi huu ndege moja iliruka kutoka upande wa pili (Ureno) ikiruka juu sana ya kiwanja cha ndege. Ilipotazamwa, haikuonekana kwa kuwa ilikuwa inaruka juu sana. Baadaye ilirudi ilikotoka.

"Kwa kweli, akasema, "japokuwa sisi watu wa Newala tunalala na kuamka, lakini hatujui nini kitatokea baadaye."

Pia akaeleza juu ya kuzidi kwa uhalifu. Akasema kuwa Serkali iliku-

wa inawarudisha makwao wale ambao walikuwa hawana kazi. Wamakonde ambao wamerudishwa kule kutoka sehemu za mijini, wamepata ustaarabu wa mijini. Kama vile kwenenda sinema na kadhalika. Pale Newala hakuna mambo kama haya. Matokeo yake ni kama uvunjaji wa maduka umezidi.

June, 24-63